# HADHIRA YA USHAIRI HURU WA KISWAHILI NI IPI?

*Joseph N. Maitaria*

**Ikisiri**

*Makala hii inaangazia mustakabali wa hadhira katika upokezi wa ushairi huru wa Kiswahili. Mwanzoni mwa miaka 1970, ushairi huu ulijitokeza kwa kasi na ulituhumiwa kwa kutozingatia arudhi za kimapokeo. Watunzi wa awali wa ushairi huu walikuwa wataalamu wa lugha na wahakiki wa fasihi; waliotoa maelezo muhimu kuhusu dhana na sifa za ushairi wa Kiswahili. Kabla ya miaka 1960, ushairi wa kimapokeo ulikuwa umesambaa na umezoewa katika jamii. Kujitokeza kwa ushairi huru kulisababisha watunzi na hadhira kugawanyika katika makundi: lile linalojinasibisha na arudhi, lile lisilojinasibisha na arudhi, na lile linalojinasibisha kwa kiasi na arudhi hizo. Katika miaka ya 1970, waliouendeleza zaidi ushairi huru walikuwa 'vijana' waliobahatika kupata elimu ya juu katika taaluma ya fasihi na walitarajia kuchangia katika ufafanuzi wa dhana na sifa za ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Swali linalofafanuliwa katika makala hii ni: kwa nini ushairi huru wa Kiswahili ni kivutio cha wataalamu wa lugha na wahakiki wa fasihi? Nadharia ya Semiotiki imetumika kufafanulia matini za lugha kama viishara na viashiria vinavyohitaji kufasiriwa. Data ya uchanganuzi ilitokana na upitiaji wa mashairi katika diwani teule za mashairi ya Kiswahili. Aidha, data nyingine ilitokana na usaili na hojaji kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na wataalamu wa lugha na fasihi.*

## Utangulizi

Katika historia ya Afrika Mashariki, ushairi wa Kiswahili umekuwa ukitumiwa katika jamii kwa miaka mingi ukilinganishwa na tanzu zingine za fasihi (Senkoro, 2011; Mulokozi, 1999). Umekuwa ni chombo cha kuwasilishia masuala muhimu katika jamii. Aidha, unawasilishwa kwa kuzingatia hali halisi katika jamii. Katika uwasilishaji, watunzi wa tungo hizi hutumia lugha ya kisanii katika muktadha wa sajili ya kishairi (Shitemi, 2010). Matukio muhimu huwasilishwa kwa kuzingatia ukweli-ubunifu katika muktadha wa falsafa ya wenyeji. Kwa kuzingatia historia ya ushairi wa Kiswahili (na hasa katika miaka ya 1950), baadhi ya tungo zilikiuka arudhi za kimapokeo. Tungo hizo zilifahamika kama mashairi guni. Katika kukabiliana na hali hii, taratibu ziliwekwa wazi, hususani katika *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (Abedi, 1954). Mwishoni mwa miaka ya 1960, mashairi huru yaliyojitokeza kwa ghafla na kwa kasi. Katika mazingira haya, wakereketwa wa mashairi ya kimapokeo walijitokeza ili kutahadharisha umma

kuhusu 'uchafuzi' uliokuwa 'ukipenyezwa' katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili. Kwa sasa, mashairi ya Kiswahili yanawasilishwa kwa kuzingatia, kutozingatia (kwa makusudi) au kuzingatia kwa kadri arudhi za kimapokeo. Mashairi hayo yana hadhira tofautitofauti kama inavyofafanuliwa katika makala hii.

**Data iliyochanguliwa na Misingi ya Nadharia**

Data ilitokana na usomaji wa mashairi yaliyohifadhiwa katika diwani za mashairi ya Kiswahili. Mashairi teule yalipata maelezo ya wasailiwa ambao ni wataalamu wa lugha na fasihi na wanafunzi wa lugha na fasihi ya Kiswahili wa vyuo vikuu. Wahojiwa walifikiwa ili kupata fasiri za kijumla kuhusu mashairi ya kimapokeo na mashairi huru ya Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki. Sababu ya kutumiwa kwa nadharia hii ni kwamba, mashairi ya Kiswahili huwasilishwa kwa miundo maalumu ya lugha na maana tarajiwa imejikita katika aina ya viashiria na viwango vya viashiriwa katika utamaduni jamii. Nadharia hii ilipata umaarufu baada ya udhaifu wa wanamiundo kubainika kuanzia miaka ya 1970. Kwa mfano, baadhi ya wanamiundo walijikita zaidi katika kuhakiki na kufafanua miundo ya lugha badala ya kubainisha uwiano uliopo baina ya matumizi ya miundo hiyo kama viishara vinavyohitaji uzingatiaji wa viwango vya viashiriwa katika utamaduni wa jamii (Peck na Coyle, 1984; Hawkes, 1977 na Pierce, 1977). Kwa mujibu wa Scholes (1982), nadharia ya Semiotiki si ngeni, bali ilidokezewa mwaka 1916 na mwanaisimu Ferdinand de Saussure. Inadai kwamba, lugha ni mfumo wa ishara - fasiriwa. Kadhalika, misingi na mihimili yake iliwekwa wazi na Pierce (1977). Kwa hivyo, kauli teule zinazotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe hutokana na utamaduni wa jamii. Nadharia ya Semiotiki ilitumiwa mwanzoni mwa miaka 1960, kupitia Roman Jacobson aliyebainisha vipengele sita vinavyohusu utaratibu unaobainika katika mawasiliano ya watu. Vipengele hivyo ni msemaji, mpokezi, muktadha, matini, utanzu na lugha inayoibainisha zaidi kwa kuzingatia viashiria vyenye yambwa na vifasiri. Mnamo mwaka 1977, Charles Pierce aliendeleza zaidi mawazo ya Jacobson (keshatajwa) kwamba; kila ishara (matini au kitendo cha kijamii) huwa vichocheo vya tafakari kwa kurejelea miktadha ya tamaduni na uhalisi wa jamii. Kinachosisitizwa ni kwamba, viashiria hujengwa kwa misingi ya kufafanuliwa na kufasiriwa. Kwa hivyo, maana inayokusudiwa hutegemea viwango vya fasiri vya mwasilishaji na mpokezi. Kwa kuzingatia ufafanuzi wa Pierce (keshatajwa), viashiria au viashiriwa vya kiistiari huakisi zaidi viwango vya maana fiche ingawa kuna haja ya kufasiri maana za kijumla (zilizo wazi) katika miundo ya maneno inayotumika. Kwa hivyo, fasiri na maana katika mashairi huweza kubainishwa katika viwango mbalimbali kutegemea viwango vya ufasiri na mielekeo ya hadhira.

**Utata katika Fasili ya Dhana ya Ushairi wa Kiswahili**

Fasili mbalimbali kuhusu dhana ya ushairi wa Kiswahili zimetolewa kwa kuzingatia mirengo ya watunzi na wahakiki wa fasihi. Miongoni mwa watunzi na wahakiki hao ni: Abedi (1954). Abdalla (1973), Massamba (1976), Kezilahabi (1979), na Mulokozi na Kahigi (1979). Wengine ni: Mayoka (1986), Chacha (1987), Mazrui (1988), Sanka (1995), Gibbe (1998), Wamitila (2008) na Senkoro (2011; 1988). Nabhany (katika Said, 2012:63) ameeleza kuwa, ushairi wa Kiswahili lazima uwe na sifa zifuatazo: bahari, kina, mshororo, mikondo, kituo, kikomo na mizani[2]. Mawazo hayo yameegemea kwenye ushairi wa kimapokeo. Ushairi ni utungo unaowasilisha mawazo kwa ufupi, kipicha na kiutafakari. Aidha, unaweza kughaniwa kwa mahadhi. Baadhi ya wataalamu wana mawazo kuwa, uwasilishaji wa ana kwa ana wa utungo huu si lazima uimbwe kwa mahadhi ya kuvutia, bali uzingatie muktadha uliosawiriwa (Wamitila, 2002; Senkoro, 1988; Kezilahabi, 1974).

Mashairi ya awali katika miaka ya kabla ya 1960 yalitungwa na yalihifadhiwa kimoyomoyo au kuandikwa kwa azma ya kughaniwa hadharani. Kuna uwezekano kuwa, hiyo ndiyo sababu ya baadhi ya watunzi awali kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo katika miaka ya 1980. Miongoni mwa watunzi hao ni S.A. Mohamed katika *Sikate Tamaa* (1980) na *Kina cha Maisha* (1984). Baadaye, mtunzi huyu alibadilisha namna ya uwasilishaji wake na kuzingatia zaidi mbinu za ushairi huru katika *Jicho la Ndani* (2002). Mtunzi huyu amelenga kukita tungo zake kwenye mwelekeo wa ushairi huru (ambao ni kivutio cha watafiti, wasomi na wahakiki wa fasihi). Mwelekeo wa mtunzi huyu umebainika kwenye beti za kwanza hadi tano shairi la ‘Arudhi’ (uk. 78):

> <u>Kina, ni cha nini kina?</u>
> …
> Zitakazonifanya kuzamia kwenye vina na kuoge~~a~~lea! (ubeti wa 1)
> <u>Mizani, kwa nini mizani?</u>
> …
> Yakayonipelekea kutisha sawiya maudhui na fani! (ubeti wa 2)
> <u>Urara, wa nini urari?</u>
> …
> Zitakazoumua umbo lis’o mshazari (ubeti wa 3)
> <u>Ubeti, kwa nini ubeti?</u>
> …
> Itakayoimbika, kwa ari kutoka kila ubeti! (ubeti wa 4)
> <u>Muwala, kwa nini muwala?</u>
> …

---

[2] Huu ni mtazamo wa baadhi ya watunzi wanaoegemea katika mashairi ya kiarudhi ya Kiswahili.

Itakayofanya muwala utiririke hadi hatima! (ubeti wa 5)

Madondoo hayo, hasa mishororo iliyopigiwa mistari, yanatumulikia kwamba, vipengele vya kina, mizani, urari, beti na muwala si mambo ya lazima katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, ni dalili kuwa, baadhi ya washairi ambao pia ni wahakiki wa fasihi wanafikiria upya kuhusu ushairi wa Kiswahili na kuukubali ushairi huru.

**Ushairi wa Kimapokeo na Ushairi Huru**

Mwishoni mwa mwaka 1960, mashairi yasiyozingatia mno arudhi za kimapokeo yalijitokeza na kupata mwanya katika ulingo wa ushairi wa Kiswahili. Kipindi hicho kilishuhudia mgogoro katika ushairi wa Kiswahili (Gromov, 2006). Kutokana na watunzi wa ushairi huru kuwa pia wataalamu wa lugha na wahakiki wa fasihi, walijihami kwa maelezo yaliyojikita katika taratibu za nadharia za lugha na fasihi. Miongoni mwa nadharia zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi huo ni Udhanaishi, Ufeministi, Udenguzi, Ubwege, Uhalisia wa Kijamaa, Ujumi Mweusi, na Uhalisia Ajabu. Baadhi ya wahakiki wasifika katika lugha na fasihi ya Kiswahili waliounga mkono mawazo ya watunzi hao ni F.E.M.K. Senkoro, S.A. Mohamed, K. Wamitila, K. wa Mutiso, J. Angira, K. Njogu na A. Mazrui. Aidha, wahakiki hao ni watunzi wasifika wa ushairi wa Kiswahili.

Washairi huru wa awali walipojitokeza, walifafanua mambo mawili ya muhimu: maana ya jumla ya ushairi na maana ya shairi la Kiswahili. Maelezo yao yalilenga kufafanua zaidi maana na dhima ya ushairi wa Kiswahili katika jamii (Njogu, 2004; Chacha, 1992; Mulokozi, 1982). Hata hivyo, walituhumiwa kuwa 'wachafuzi' wa ushairi wa kimapokeo. Watunzi wa ushairi wa kiarudhi walitaka kuhifadhi kaida zilizofahamika kimapokeo. Kutokana na makabiliano hayo, kila kundi lilijitahidi kunoa zaidi kunga za uwasilishaji katika tungo zao. Mifano ya washairi waliozingatia mno arudhi za kimapokeo ni Wallah (1988), Karama (1985), Mbega (1984), Amana (1983), Snow-White (1974), Abdalla (1973) na Nassir (1971). Kadhalika, mifano ya washairi huru ni Wamitila (2004 – mhar.) Kezilahabi (2008; 1974), wa Mberia (2001), Mohamed (2002). Kimtindo, mashairi hayo yanaweza kuchukuliwa kuwa ya pande mbili ya sarafu moja; kimaudhui yanashabihiana (Senkoro, 1988; Mulokozi na Kahigi, 1979). Mashairi hayo yanadhihirisha weledi wa kiutunzi wa watunzi hao.

**Maumbo na Miundo katika Mashairi Huru**

Katika muktadha wa Afrika ya Mashariki, mashairi huru yalikuja kwa ghafla kabla ya hadhira haijatayarishwa wala kuelekezwa kuhusu upokezi wa tungo hizi. Ushairi huru unawasilishwa kwa maumbo na miundo mbalimbali kama vile michoro na

picha ya vitu halisi. Mfano wa mashairi hayo ni 'Mruko wa Nyuki' katika *Bara Jingine*. Shairi hili limewasilishwa kwa taswira ya kiwima kwa kuzingatia neno mojamoja, ambapo katikati kuna umbo la panda: kushoto na kulia. Sehemu ya kulia, kuna maneno yamepangwa katika mstari mmoja kama ilivyo katika sehemu ya mwanzo. Sehemu ya kushoto, neno 'liliporomoka' limewasilishwa kwa taswira halisi ya tukio hilo kama inavyodhihirika katika shairi hili:

...
panda
tatizi,
...
njia
Moja
iliingia kulia
nyingine ikapitia
kushoto baadhi
yetu tulisafiria
kushoto wengine
walifuata kulia
…
i po
li ro ka
mo
waliokuwemo walijiunga
na
njia
ya
kulia

… wa Mberia (2001: 20-25).

Nalo shairi la 'Nyumba' (uk. 17) katika *Mchezo wa Karata* (wa Mberia, 1997) limewasilishwa kwa umbile la paa la nyumba. Katika sehemu ya kushoto na kulia kuna umbo la kuta, chini yake maneno yamepangwa kiulalo (ili kuunda sakafu). Kiumbo, shairi hili limevishwa umbo la kibanda. Huu ni mfano mmojawapo wa mashairi yaliyowasilishwa kwa maumbo ya taswira inayoonekana. Mifano mingine ni: 'Mafahali Wapigana' katika *Kichomi* (Kezilahabi, 1974:5). Shairi hilo

limewasilishwa kwa taswira ya mawazoni na linaposomwa kimyakimya au kwa sauti, msomaji huweza kujiundia taswira ya tukio linalokusudiwa. Shairi hili limesawiri mafahali wawili ‘wenye matumbo’ wanaopigana na watu waliokonda wanashangilia. Aliyeibuka mshindi amesimama kwenye kichuguu, anajigamba huku akinyooshea kidole hadhira inayosikiliza. Kutokana na maneno yaliyotumiwa, msomaji anajiundia taswira kamili kuhusu tukio hilo. Shairi hili limewasilishwa kwenye ubeti wa kwanza ifuatavyo:

> Mafahali wenye matumbo wanapigana.
> Chini, chini, chini zaidi
> Mpaka vichwa vyao vinagusana.
> Halafu watazamaji wakondefu
> Wanaanza kupiga kelele.
> Haya! Haya! Machakulo* haya!
> …
> Vumbi kuisha, mshindi amekwishakimbia.
> Mshindi juu ya kichuguu amekaa,
> Akionesha kidole kimoja
> Mchwa ndio askari (uk. 5)

Taswira katika dondoo hilo inaweza kuundwa kwenye bongo za hadhira kutokana na fasili na tafakari ya msomaji. Hii ni kinyume na mashairi ya Kithaka wa Mberia kama ilivyodokezwa hapo awali. Kulingana na Gromov (2006), mtindo huu upo na unabainika pia katika mashairi ya kimapokeo. Hata hivyo, katika mashairi huru unajitokeza kwa uwazi zaidi. Kwa maelezo zaidi juu ya hili, tazama shairi la ‘Dau haliendi’ katika *Natala* (wa Mberia, 1997:32).

Aghalabu, ushairi huru wa Kiswahili huwasilishwa kwa miundo inayojikita kwenye viwango vya isimu kama vile mofolojia, mantiki, na sintaksia. Miundo hiyo ni ya makusudi kwa azma ya kujenga ridhimu katika tungo hizo. Mifano hiyo inabainika zaidi katika ‘Geuko Twataka’ (*Mageuzi*, uk.31), ‘Mimi Mtupu’ na ‘Kusimamia Guu Moja’ (*Jicho La Ndani*, uk. 157, 165-166, mtawalia), ‘Bara Jingine’ (*Bara Jingine*, uk. 10-16). Katika shairi la ‘Bara Jingine’, msomaji huelekezwa kuzingatia marudio ya baadhi ya vipande vya mishororo au mistari ya ‘Bara ambapo’. Kulingana na Parry (1971), marudio ya kauli na maneno teule ni za uelekezaji na uashiriaji wa mwanzo, hoja ngeni au mianzo ya beti za ndani kwa ndani. Isitoshe, usomaji wa shairi hili umedhibitiwa kwa herufi kubwa na viakifishi kama vile kishangao (!), kiulizi (?), kituo (.), ritifaa (‘), doti (...), alama usemi (“ ”), koloni (:), na kikomo au koma [,]. Katika ushairi wa kimapokeo matumizi hayo yanaweza kubashiriwa kwa kuzingatia vina vya ndani (ukwapi) na vina vya nje (utao) vinavyotiririka, pamoja na idadi maalumu ya mizani katika mishororo (Maitaria, 2017b). Kuhusu usomaji wa kazi za fasihi, Fish (1980) na Iser (1974) wameeleza kuwa, kuna usomaji wa

aina mbili: ule unaosisitiza mawazo ya awali yanayoeleweka kwa urahisi na ule unaochochea usomaji wa kiutafakari. Mashairi huru ya Kiswahili yanaposomwa bila ya kutafakari, yanaweza kutolewa kauli za kijumla zisizo na mantiki. Maumbo na miundo iliyotumika katika ushairi huu huhitaji utafiti na usomaji wa kiuhakiki, hasa kwa watafiti na wasomi wa ngazi za juu.

**Sifa Bainifu za Mashairi Huru**

Kwa sasa, mashairi huru yanatungwa katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili. Jambo linalotatiza ni jinsi ya kutambua 'kwa wepesi' kunga zinazotumiwa katika ushairi huu. Kila utungo wa fasihi huzingatia kanuni mahsusi katika uwasilishaji wake (Maitaria, 2017a). Vipengele teule na taratibu zinazotumika katika uwasilishaji wake si bayana kwa hadhira pana. Sababu hapa ni kwamba, baadhi ya mashairi hayo yanahitaji zaidi ujuzi wa kiisimu na wa kinadharia. Kabla na hadi mwishoni mwa miaka ya 1960, kulikuwa na tahakiki chache za ushairi wa Kiswahili. Tahakiki hizo ziligusia zaidi ushairi wa kimapokeo, ushairi huru haukugusiwa kwa kina.

Kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1970, sifa za kijumla kuhusu ushairi huu zimejitokeza katika dibaji na tangulizi za baadhi ya diwani zilizokuwepo. Miongoni mwazo ni *Wasakatonge* (Khatib, 2003), *Jicho la Ndani* (Mohamed, 2002), *Chembe cha Moyo* (Mazrui, 1988), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Mulokozi na Kahigi, 1979), *Kichomi* na *Dhifa* (Kezilahabi, 1974; 2008, mtawalia), pamoja na *Tamthilia ya Maisha* (Wamitila, 2005 – mhar.). Kwenye kurasa za mwanzo katika diwani hizo, kuna fafanuzi za maana ya ushairi huru wa Kiswahili na maelezo mafupi kuhusu fani zilizohusishwa.

Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1970 wahakiki wa fasihi wametoa maelezo muhimu kuhusu sifa za ushairi huru. Miongoni mwao ni: F.E.M.K. Senkoro, K.W. Wamitila, K. Njogu, A.G. Gibbe, M. Mbatiah, S.M. Sanka, E. Zubkova-Bertoncini, R.M. Wafula na M.D. Gromov. Kupitia maelezo yao, baadhi ya sifa za ushairi huru zimebainishwa kama vile: matumizi ya taswira dhahiri au ya kimawazo, mpangilio unaweza kuwa au usiwe maalumu kutegemeana na hisi na mawazo, ridhimu kutegemeana na hali na tukio linalowasilishwa, pamoja na uelekezi wa usomaji kupitia matumizi ya viakifishi. Sifa hizo si bayana kama ilivyo katika ushairi wa kimapokeo. Sifa hizo zinadhihirika katika baadhi ya mashairi ya Kithaka wa Mberia katika *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001).

Aidha, kuna mashairi yanayowasilishwa kwa taswira ya kimawazo. Mashairi hayo yanapatikana katika machapisho ya: *Mageuzi* (K.K. Kahigi, 2015), *Wasakatonge* (M.S. Khatib, 2003), *Dhifa*, *Kichomi*, na *Karibu Ndani* (E. Kezilahabi, 2008; 1974; na 1988, mtawalia) pamoja na *Mashairi ya Kisasa* na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (M.M. Mulokozi na K.K. Kahigi, 1973; na 1979, mtawalia). Aidha, mitindo ya

uwasilishaji wa mashairi hayo inashabihiana na ile inayopatikana katika mashairi simulizi. Tungo hizi zina taratibu zake. Taratibu hizo hudokezwa kwa ujumla katika vikao rasmi vya wataalamu na wadau wa fasihi (kama vile katika mihadhara ya fasihi katika vyuo vikuu na makongamano ya kitaifa na kimataifa). Hata hivyo, hadhira pana (nje ya wataalamu hao) haielewi taratibu hizo, ambapo hazina kubwa ya ushairi huru imehifadhiwa katika diwani chache ambazo hazipatikani kwa urahisi, na zinapopatikana huwa ghali.

**Uhalisi-Dhahania katika Ushairi Huru wa Kiswahili**

Masuala yanayowasilishwa katika fasihi ni yale yanayooana na uhalisi wa maisha na tajiriba ya watu (Njogu, 2004; Mulokozi, 1982). Mathalani, ushairi wa kimapokeo umekuwa ukihusishwa moja kwa moja na yale yanayotendeka katika jamii. Ijapokuwa ushairi huru unaangazia masuala yayo hayo, maelezo na fafanuzi zinazotolewa ni za kifalsafa na kinadharia. Kwa hivyo, jumbe zinazowasilishwa zina fasiri nyingi zinazohusisha 'kweli iliyopo' na 'kweli ya kidhahania'. Katika kufafanua dhana ya kweli ya kifasihi, Tolstoy (1975) ameelezea mshabaha unaojitokeza katika pande mbili: kwamba, linaloshughulikiwa na msanii linaweza kuwa katika uwezekano au lisiwe katika uwezekano. Kwa mantiki hii, mtunzi ana uhuru kuwasilisha ujumbe kwa njia mojawapo au zote mbili.

Mbinu zinazotumika katika uwasilishaji wa jumbe katika mashairi huru zimefichwa kiufundi katika maana na mpangilio wa makusudi wa maneno. Fasili hizo huhitaji utaalamu wa lugha na uhakiki wa fasihi. Masuala ya kipaumbele katika ushairi huru yanazingatia usawiri wa yale yaliyotokea ili kufafanua yale yanayoshuhudiwa na utabiri wa kimaono. Isitoshe, mawazo na maono yanaweza kuwa ya kibinafsi (Harland, 1999). Baadhi ya mashairi huru yana mwelekeo huo kupitia kauli zinazotumiwa. Mifano inapatikana katika kauli zilizomo kwenye shairi la 'Bara Jingine' katika *Bara Jingine* (2001:10-16). Kauli hizo ni: 'Ndoto yangu ni tamu', 'Kesho ambapo' na 'Bara ambapo'. Kauli hizo zinazingatia yale yanayowezekana japo hayapo. Jambo linalosisitizwa hapa ni thamani ya kitu kilichokuwapo na kupuuzwa kwa kuthamini kile kisichofahamika. Katika muktadha huu inaweza kuelezwa kuwa, ushairi huru umeingia kwa ghafla na kishindo kwa hadhira ya ushairi wa Kiswahili. Tukio kama hilo linapotokea, hadhira inaweza kujiuliza maswali na kujitolea majibu ya kubahatisha (Mathiora & Mudachi, 2007). Aidha, tungo za fasihi zinazofasiriwa kwa kuzingatia tajriba ya wanajamii, huwa maarufu na hukubaliwa na hadhira (Pierce, keshatajwa). Aidha, tungo hizo hudumu na huchukuliwa kama kazi bora. Baadhi ya tungo hizo ni zile zilizowasilishwa na Abdilatif Abdalla, Shaaban Robert, Muyaka bin Haji Al-Ghasaniy, Mwana Kupona, na Sayyid Abdalla Nassir.

Maudhui katika tungo za ushairi wa kiarudhi yamekuwa yakiwasilishwa kwa kuzingatia zaidi tasfida. Kinyume na hayo, ushairi huru umekuwa ukiwasilisha mawazo kwa makali ya lugha na, wakati mwingine, masuala muhimu katika jamii yamekuwa yanakejeliwa. Katika diwani ya *Kichomi* (Kezilahabi, 1974) kuna mashairi kama vile: 'Bikira mwenye Huzuni' (uk. 3) na 'Nimechoka' (kur. 34-35). Kwa mtazamo wa utamaduni wa Kiafrika, ubikra na ndoa ni ishara ya malezi mema kwa vijana kutoka kwa wazazi. Kadhalika, wasichana walijivunia ubikra hadi wanapoolewa, huku ikizingatiwa kuwa suala la ndoa ni muhimu katika jamii. Masuala haya yamejengewa kejeli kwa makusudi: ubikra kuwa 'adhabu' na ndoa kuwa 'jambo la kawaida'. Mfano unapatikana katika ubeti wa kwanza na wa tano kama ifuatavyo:

Miaka kumi ya uchovu
Mapenzini na msichana
Aliyeishi pangoni
Ilikuwa imepita kwa huzuni.

Ndoa ni jambo la kawaida
Au ujuzi fulani usojulikana
Ambao hausahauliki
Na akili za kibinadamu? (uk. 5)

Aidha, katika shairi la 'Nimechoka' kuna mhusika ambaye anateseka. Wapita njia wanamtazama bila chembe ya hisia wala kumwonea huruma aliyepatwa na janga. Hata baba mzazi yumo kundi hilo, kwa pamoja, wanakebehi na wanafurahia. Hadhira ya shairi hili inajengewa ukatili wa aina fulani. Katika utamaduni wa Kiafrika, wanajamii wanatarajiwa kusaidiana. Kadhalika, haiyumkiniki mtu anayeteseka kufurahia dhiki kama inavyowasilishwa katika ubeti wa nane kama ifuatavyo:

Ninaendelea kuning'inia. Nimechoka. Mikono
Inaniuma; hatari ya vitimbo. Vinacheka. Wanasali
Sasa wanaimba. Sitaki nyimbo zao; maana
Mimi bado nimening'inia na vitimbo having'oki
Lakini polepole ninaanza kutabasamu.
Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka
Kichomi kimenipata na sijadondoka (uk. 34).

Mawazo hayo yaliwasilishwa katika baadhi ya mashairi huru. Kwa mfano, tunaona wagonjwa hawapewi ugua pole bali wanashutumiwa na wanalaumiwa kwa maradhi yao katika shairi la 'Nakumbuka Ulivyokuwa' *Bara Jingine* (2001:10-16). Zaidi, ~~kuna~~ wahusika wanaosifiwa ni wachawi katika shairi la 'Ahadi ya Mchawi' *Mashairi ya Kisasa* (1973:19). Suluhu inayopendekezwa ni ya uasi kwa kuzingatia 'hasira' au nguvu za kibinafsi katika shairi la 'Hasira Hasara?' *Chembe cha Moyo*

(1988:23). Ingawa kauli hizo zina chembe za kweli kuhusu maisha, ufafanuzi wa ukweli huo si wazi kwa kuzingatia uwezo wa kiuchanganuzi wa hadhira pana katika jamii.

**Harakati za Makusudi katika Kuuvumisha Ushairi wa Kimapokeo**

Katika magazeti ya Kiswahili kwa sasa katika mataifa ya Afrika Mashariki kuna ithibati ya wachangiaji wa mashairi huru. Kwa mfano, nchini Kenya kuna gazeti moja la Kiswahili, *Taifa Leo*, na nchini Tanzania kuna magazeti ya Kiswahili kama vile *Majira*, *Mtanzania*, *Mwananchi*, *Nipashe*, *Mzalendo* na *Uhuru*. Katika magazeti hayo, mashairi yanayochapukiwa zaidi ni yale ya kiarudhi. Mashairi huru huwa nadra kupatikana katika safu za magazeti hayo; yanapojitokeza huwa machache na hayana mvuto wa kiujumi. Wanaoshiriki katika safu hizo hupata fursa ya kuwasilisha hisi zao kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi.

Baadhi ya mashairi hayo yanapatikana katika gazeti la *Taifa Leo*, siku ya Jumamosi katika safu ya 'Ushairi Wetu' (uk.25) na Jumapili, safu ya 'Sokomoko' (uk.21). Isitoshe, kila mwaka Wizara ya Elimu nchini Kenya huandaa matamasha ya muziki kwa wanafunzi. Mashairi ya kiarudhi ndiyo yanayotumiwa mno katika matamasha hayo.

Kwa upande wa idhaa za radio, nchini Kenya kuna *Radio Citizen, Radio Maisha* na *Kenya Broadcasting Corporation*. Nchini Tanzania kuna *Tanzania Broadcasting Corporation* na *Radio Free Africa*. Runinga za mashirika hayo pia hupeperusha vipindi maalumu vya mashairi yanayozingatia arudhi. Aghalabu, mashairi hayo hutumiwa kuwa 'vijipumuo na vijiliwazo' au vitumbuizo kwa wasikilizaji. Kulingana na Ngolo (2011) na Massamba (1976), watunzi wa mashairi ya kiarudhi hawashurutishwi bali huwasilisha tungo kwa raha zao. Isitoshe, katika matbaa ni diwani chache za mashairi huru huchapishwa.

**Uelekezaji wa Kijumla**

Watunzi wa ushairi huru walikuwa na ari ya kubainisha vipengele muhimu katika ushairi wa Kiswahili. Ubainishaji huo ulijikita katika yale waliyoyapata katika usomi wao wa fasihi linganishi za kimataifa. Katika miaka ya 1960 hadi 1980, pande hizi mbili zilijihami kwa hoja zilizowasilishwa kwa hasira. Mawazo ya washairi huru yalikuwa ya kuelekeza lakini yalikuja kwa ghafla. Ingawa wataalamu na watunzi wa awali wa ushairi huru walikuwa na mawazo muhimu ya kuufunua upande mwingine wa ushairi wa kiarudhi, hawakuzingatia subira. Walieleza kuwa, vina na mizani si vipengele vya lazima katika ushairi wa Kiswahili (Momanyi na Maitaria, 2018; Sanka, 1995; Mulokozi, 1982).

Kutokana na ukosefu wa subira, waanzilishi wa ushairi huru (E. Kezilahabi, K.K. Kahigi na M.M. Mulokozi) walipagazwa majina ya ‘Watundu Watatu’ wa ‘Mlimani’. Watatu hawa walituhumiwa kuleta ‘sumu’ na kuingilia ‘ngome takatifu ya jadi’ ya ushairi wa Kiswahili wa kimapokeo. M’Ngaruthi (2012) na Kezilahabi (1983) wanashikilia kuwa, mgongano kati ya wanamapokeo na wanamapinduzi haukuweza kuepukwa. Je, washairi huru walitumia mikakati gani katika kufafanua hoja zao? Mwongozo mwafaka ungekuwa kushiriki majadiliano ambayo yangeleta maridhiano. Kuhusu suala hili, Mzee Mahmoud Ahmed Abdul Kadir (almaarufu *Ustadhi Mao*) ambaye ni mtunzi maarufu kutoka Lamu, ameeleza kuwa: washairi wa kimapokeo wanatambua kuwapo kwa washairi huru na umaarufu wa tungo hizo unatokana na kutozingatia baadhi ya arudhi za kimapokeo[3]. Kulingana na Richard M. Wafula[4], watunzi na wahakiki wa ushairi huru wa Kiswahili wamechangia katika kufafanua zaidi vijenzi muhimu vinavyotumiwa kuuwasilishia ushairi wa Kiswahili. Maoni ya Kithaka wa Mberia[5] ni kwamba, ushairi wa Kiswahili hauna ulazima wa kuimbika kwa mahadhi yanayolingana bali kwa kuzingatia mawazo na hisi zinazowasilishwa. Kwa kuzingatia mawazo hayo, ushairi huru una taratibu zake na unachangia katika kuuendeza zaidi ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Kwa hivyo, mgororo katika ushairi wa Kiswahili haukupaswa kuwapo katika miaka ya 1970 na 1980.

Katika historia ya ushairi wa Kiswahili hadi miaka 1960 (na kwa kiasi fulani hadi sasa) ushairi wa kiarudhi umekuwa ukifahamika kuwa ni ‘himaya ya umma’. Wanamapokeo hawakuwa wanakataa mabadiliko bali hitilafu ilitokana na dharura iliyopandwa na washairi huru. Walipobaini athari ya kauli zao katika miaka ya 1980, baadhi ya watunzi walikuwa tayari wameanza kutunga tungo bila kuzingatia mihimili ya ushairi huru. Chuki na tuhuma tayari zilikuwa zimekwishapandwa, kila kikundi kikivutia upande wake. Kutokana na elimu ya juu ambayo washairi huru

[3]Haya yanatokana na mahojiano ya msanii huyu yanayopatikana katika safu ya ‘Gwiji wetu’ kwenye Gazeti la *Taifa Leo* (tarehe 4.3.2015, uk. 17). Mzee Mahmoud Ahmed Abdul Kadir anakiri kuwa yeye amekuwa akitunga mashairi ya Kiswahili kwa miaka mingi kwa kuzingatia arudhi za kimapokeo. Ushairi huru pia umepata wafuasi kutokana na kushirikishwa kwa kiwango fulani cha arudhi katika uwasilishaji wake. Alizaliwa Februari 1952.

[4]Mawazo haya yametokana na mahojiano yetu na mtaalamu huyu ya tarehe 9.6.2017. Yeye ni mtaalamu wa fasihi linganishi, mhakiki wa fasihi na mhadhiri katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

[5]Mawazo haya yametokana na mahojiano yetu na mtaalamu huyu katika Kongamano la CHAKAMA, Dodoma, Tanzania tarehe 23.11.2017. Yeye ni mtaalamu wa lugha na Isimu, mtunzi wa mashairi huru na Profesa katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Baadhi ya diwani zake ni *Rangi ya Anga* (2014), *Msimu wa Tisa* (2007), *Radio na mwezi* (2005), *Bara Jingine* (2001) na *Mchezo wa Karata* (1997).

waliipata ughaibuni, walitaka sauti yao kusikika. Hilo halikuridhiwa, kwani waliwafanya washairi wa kimapokeo kuchukua hatua ya dharura ya kuwashikisha adabu 'watoto watundu' hao. Walichukua hatua hiyo ili 'sumu' isiweze kusambaa na kuwaathiri 'watoto watiifu' katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili. Ushairi uliozingatia zaidi arudhi ulikuwa kama sanaa inayoumbiwa watu fulani. Waliotoka nje hawakuruhusiwa kuingia katika ngome hiyo kabla ya kuelekezwa kwenye mizungu ya sanaa hii. Walioonjeshwa mawazo hayo, wanaweza kufananishwa na tunda linaloning'inia lisijulikane iwapo limeiva au ni tosa. Baadhi ya watunzi wa baadaye hawakuwa na waelekezaji; waliachwa kupiga mbizi katika bahari wasiofahamu kina chake. Hadhira nayo haikupata maelekezo mwafaka katika usomaji wao; baadhi wameachwa kucheza ngoma wasiyoimaizi vilivyo. Waliobobea katika sanaa ya ushairi huru ni walewale. Isitoshe, watunzi hao walikuwa na namna tofauti za uwasilishaji. Kwa mfano, wa Mberia amezingatia zaidi mashairi ya kimchoro (taswira za kimaono), ilihali akina E. Kezilahabi, K.K. Kahigi, S.A. Mohamed na A. Mazrui wamezingatia zaidi taswira zinazoundwa kwa maneno. Washairi huru walianza kwa kutunga mashairi na muda mrefu ndipo makala za tahakiki kuhusu ushairi huo zikaanza kuchapishwa katika majarida ya *Kioo cha Lugha*, *Kiswahili* na *Mulika.* Kadhalika, baadhi ya tahakiki za ushairi zilianza kujitokeza kama vile *Nadharia: Tahakiki ya Ushairi wa Kiswahili* (Senkoro, 1988). Isitoshe, katika tatanguli za diwani za watunzi wa ushairi huru kuna fafanuzi fupi kuhusu ushairi huru kama inavyobainika katika *Kunga za Ushairi na Diwani yetu* (1979). Waliochukuliwa kuwa ni 'Baba' wa ushairi huru katika miaka ya 1970, kwa sasa ni 'wazee'. Watunzi wenye nia ya kuelekezwa wameachwa wakiwa wachanga wakitambaa; hawajainuka wala kutembea[6]. Wafuasi wa baadaye wa ushairi huu wanaishi katika kivuli cha waanzilishi.

**Ushairi Huru kama Kanzi ya Data ya Utafiti**

Kwa kuzingatia kasi ya watunzi wa ushairi huru wa Kiswahili katika miaka ya 1960 hadi sasa, baadhi ya watafiti wamepata uwanja wa ulinganishaji na utofautishaji wa mashairi katika jamii mbalimbali. Kutokana na namna mashairi ya Kiswahili yanavyowasilishwa kwa mitindo tofautitofauti, kumekuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu masuala ya kiutunzi na usomaji wa kimkakati. Katika muktadha wa ushairi huru, vigezo vilivyokuwa vikitumiwa kwa ujumla vinaweza kutazamwa upya ili kuuainisha zaidi kwa utaratibu unaozingatia mbinu za kisayansi. Ijapokuwa ushairi huru wa Kiswahili ulijitokeza wazi katika miaka ya 1960, tena kwa sura au maumbo ya nje yasiyoeleweka na yasiyopendeza, kupendeza kwake husitiriwa kwa fani na uwasilishaji wa kiufundi wa ndani kwa ndani katika mashairi hayo. Katika

[6]Ithibati, ni vyema kutazama baadhi ya mashairi huru machache yanayochapishwa katika safu ya magazeti ya Kiswahili nchini Kenya kama vile *Taifa Jumamosi* na *Taifa Jumapili*.

mazingira haya, ushairi wa Kiswahili utakuwa umevuka mipaka ya kuchukuliwa kiujumla na kushughulikiwa kitaaluma zaidi. Hii ni kwa sababu watunzi watakuwa wamefunuliwa namna mbalimbali za kuufahamu zaidi ushairi huo kutokana na sifa za kisayansi. Kwa sasa, ushairi wa Kiswahili unafafanuliwa kwa vigezo vilivyozalika kutokana na uchunguzi wa kisayansi. Ingawa safari ya washairi huru ilikuwa ya kukatisha tamaa kwa kutopigiwa upatu na wakereketwa wa ushairi wa kiarudhi kwa mawazo kwamba, 'ushairi wao' umehujumiwa au 'umetiwa najisi', ndoto yao haikuyeyuka. Walisonga mbele kwa kusema 'atakayesikia na asikie' na 'asiyetaka kusikia asisikie'. Misimamo hiyo ipo na ushairi huru una hadhira yake.

## Hitimisho

Ushairi huru na ushairi wa kimapokeo ni tungo mbili za sarafu moja. Watunzi wa tungo hizo wanahitaji kuwa na sauti moja ya kuchangiana. Kimantiki, ugeni kwa mara ya kwanza unaogofya na unatuhumiwa. Wapenzi wa ushairi wa Kiswahili wajitolee katika usomaji wa kiuhakiki na kiutafiti ili kuweza kufafanua zaidi misingi inayotumika katika uwasilishaji wa tungo za ushairi huru. Matokeo hayo yatabainisha zaidi sifa za msingi katika ushairi, la sivyo tuhuma zinaweza kuendelezwa miongoni mwa watunzi na hadhira. Tofauti za kiutunzi katika makundi haya zinaweza kushirikishwa katika kufafanulia vipengele vya ushairi wa Kiswahili. Makundi haya ni sura mbili za sarafu moja katika kuujenga ushairi wa Kiswahili.

Ingawa waanzilishi wa ushairi huru walikuwa wenye nia njema katika kuuchangia ushairi wa Kiswahili, mwafaka huo utafikiwa iwapo hadhira pana itajengewa mazingira ya kukumbatia ushairi huu. Taratibu zinazotumika katika uwasilishaji wa ushairi huru wa Kiswahili zinahitaji kuwa bayana kwa watunzi na hadhira ya ushairi wa Kiswahili. Kadhalika, mashairi huru yanahitaji kujengewa mazingira ya makusudi katika kupigiwa upatu kupitia vyombo vya habari kama vile: vipindi vya radio, katika safu za magazeti ya Kiswahili.

## Marejeleo

Abdalla, A. (1973). *Diwani ya Sauti ya Dhiki*. Nairobi: OUP.

Abedi, K.A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: KLB.

Barber, K. (1997). "Views of the Field" katika Barber (Mhar.) *Readings in African Popular Culture*. Oxford: James Currey.

Chacha, C.N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi*. Dar es Salaam: TUKI

Chacha, C.N. (1987). "Meaning and Interpretation of Swahili Poetry: A Portrayal of Changing Society", Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa).

De Saussure, F. (1916). *Course de Linguistique Générale*. Paris: Payot. (Tafsiri ya Kiingereza -1959 - *Course in General Linguistics*. New York: McGraw-Hill).

Gibbe, A.G. (1998). "Sajili ya Ushairi" katika *Mwongozo wa Ushairi.* Na. I. Mashairi ya Tarbia. SEKUKI. kur: 8-17.

Gromov, M.D. (2006). "The Question of Kiswahili Style Again? The Poetry of Kithaka wa Mberia" katika *KISWAHILI Juz. la 69.* Dar es Salaam: TUKI. kur. 109-126.

Harland, R. (1999). *Literary Theory from Plato to Barthes: An Introductory History*. New York: St. Martin's Press.

Hawkes, T. (1977). *The Structuralism and Semiotics*. London: Methuen.

Iser, W. (1974). *The Implied Reader.* Baltimore: Johns Hopkins University Press.

Kahigi, K.K. (1975). "Ushairi: Mtazamo wa Kisayansi." katika *Kiswahili* Juz. 45/1 Dar es Salaam: TUKI. kur. 35-54.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.

Kezilahabi, E. (1983). "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili" katika *Makala ya Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 144-163.

Khatib, M.S. (2003). *Wasakatonge.* Dar es Salaam: OUP.

M'Ngaruthi, T.K. (2012). *Miale ya Mashariki: Mashairi na Mwongozo wa Uchambuzi.* Ontario: Nsemia Inc. Publishers

Maitaria, J.N. (2017b). "Dhima ya Viakifishi katika Ushairi Huru wa Kiswahili" katika Kandagor, M.M. na wenzake (wahr.) *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja.* Eldoret: Moi University Press. kur. 1-15.

Maitaria, J.N. (2017a). "Ushairi kama Chombo cha Kuelimishia Jamii kuhusu Utamaduni: Mfano wa Ushairi Unaotumia Methali" katika Kandagor, M.M. na wenzake (wahr.) *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja.* Eldoret: Moi University Press. kur. 131-146.

Massamba, D.P.B. (1976). "Utangulizi" katika *Diwani ya Massamba*. Nairobi: Nelson East Africa.

Mathiora, J. na C. Mudachi (2007). *Reviving Poetry: Poetry Handbook for Secondary Students.* Nairobi Focus Pblishers Ltd.

Mayoka, J. (1977). "Vina na Mizani ni Uti wa Mgongo wa Ushairi" katika MULIKA Na. 9, Dar es Salaam: TUKI. kur. 3-12.

Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka.* Dar es Salaam: TPH.

Mazrui, A. (1988). "Utangulizi" katika *Chembe cha Moyo.* Nairobi: EAE P.

Mohamed, S.A. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Nairobi: Evans Brothers Ltd.

Mohamed, S.A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn.

Momanyi, C. & J.N. Maitaria (2018). "Ushairi wa Kiswahili kama Chombo cha Utetezi wa Mwanamke: Mwangwi wa Jana au Uhalisi wa Leo?" katika Omari, S & Samwel, M. (wahr.) *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili kwa Heshima ya Prof. M.M. Mulokozi*. Dar es Salaam: TATAKI, kur. 375-402.

Mulokozi M.M. na K.K. Kahigi (1973). *Mashairi ya Kisasa.* Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi M.M. na K.K. Kahigi (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu.* Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M.M. (1982). "Protest and Resistance in Kiswahili 1600-1985" katika *Kiswahili,* Juz. 49/1, kur. 25-54

Mulokozi, M.M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Ngolo, E.K. (2011). "Mabadiliko ya Kimtindo katika Ushairi wa Said A. Mohamed", Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa).

Njogu, K. (2004). *Reading Poetry as Dialogue.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Parry, A. (1971). The Making of the Homeric Verse: The Collected Papers of Milman Parry. Oxford: Clarendon.

Peck, J. na Coyle, M. (1984). *How to Study Literature, Literary terms and Criticisms*. London: Macmillan Educational Books Ltd.

Pierce, C. (1977). *Semiotics and Significs*. Bloomington: Indiana University Press.

Sanka, S.M. (1995). "Dhana ya Umapokeo na Usasa katika Ushairi wa Kiswahili" katika *Kioo cha Lugha*, Juz. la 1, Na. 2: kur. 74-80. Dar es salaam: TUKI

Scholes, R. (1982). *Semiotics and Interpretation*. New Haven: Yale University Press.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi: Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi Kitabu cha Kwanza.* Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Shitemi, N.L. (2010). *Ushairi Kabla ya Karne ya Ishirini.* Eldoret: Moi University Press

Tolstoy, L. (1975). *What is Art?* Aylmer, M. (Mtaf.). London: OUP

wa Mberia, K. (2001). *Bara Jingine.* Nairobi: Marimba Publication Ltd.

Wafula, R.M. na K. Njogu (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi.* Nairobi: JKF

Walibora, K. (2007). (Mhar). "Utangulizi" katika Walibora, K. (Mhar.) *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix.

Wamitila, K.W. (2002). "Utangulizi" katika Mohamed, S. A. *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~Muwa Publishers.